


SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



KUTAFUTA VITU VINAVYOTENGENEZA NYOTA KATIKA ULIMWENGU WETU MKONGWE WENYE VUMBI



Ulimwengu una umri wa mabilioni ya miaka. Kama ilivyo kwa vitu vikuukuu, nao pia umezingirwa na vumbi. Lakini vumbi liliopo ulimwenguni ni tofauti kabisa na lile linalopatikana nyumbani mwako. Vumbi lilipo Ulimwenguni limetengenezwa kwa chembe chembe ndogo sana, ndogo kuzidi hata unene wa unywele wa binadamu, ambazo huelea ulimwenguni baina ya nyota.

Wanaastronomia walikuwa wanalichukulia vumbi hili kama kikwazo. Kuani huzuia mwanga kutoka katika vitu vilivypo ulimwenguni, na kuufanya ulimwengu uonekane wenye giza kubwa na kuficha vitu vingi nya kuvutia.

Lakini kila wingu la vumbi linao wigo wa rangi ya fedha. Wanaastronomia walipoanza kutumia kamera maalumu kuutazama ulimwengu katika Infrared (mwanga ambao macho yetu hayawesi kuuhiisi), walitambua kwamba wanaweza kuyaona mavumbi yakig'aa .

Hii ni bahati, kuani kuna sababu nyingi muhimu za kuyasoma mavumbi haya. Vumbi ni kitu ambacho kimetengeneza binadamu, sayari za miamba na nyota nyingine!

Mavumbi ya ulimwenguni yanatengenezwa baina ya nyota sambamba na vitu vingine vavyoitwa molekyuli (chembe chembe zenye elementi, mbili au zaidi).

Kwa bahati mbaya, baadhi ya nyota hufikia kikomo cha maisha yake kwa namna ya ajabu – kwa mlipuko ang'avi ambao huweza kumulika mabilioni ya nyota. Hili likiteka, chembe chembe zote za vumbi ndani ya nyota huharibiwa.

Hili ndilo liliowashangaza wanasayansi hivi karibuni, walipogundua chembe chembe ndogo za mavumbi na molekyuli kwenye mabaki ya nyota iligolipuka!

Nyota waliyokuwa wakiichunguza ililipuka miaka 30 iliopita. Baada ya muda kupita mabaki yake yalipoa na hata kutengeneza molekyuli mpya kutoka katika maada zilikuwa zimeitengeneza nyota hiyo. Matokeo yake ni mfano wa kiwanda bora cha kuzalisha vumbi.

Hii ni taarifa nzuri, kama mtu kuibuka kutoka kwenye majivu, ndivyo nyota zilizokufa hupelekea kutengenezwa kwa nyota mpya, sayari na labda hata maisha ya aina tofauti tofauti!

COOL FACT

Nusu ya mwanga utokao ulimwenguni hufichwa kuyafikia macho ya mwanadamu kutokana na mavumbi yaliyopo ulimwengui! Kwa bahati nzuri, tumetengeneza kamera maalumu na darubini ambazo zinaweza kuudhihirisha mwanga huu uliofichwa.



More information about EU-UNAWE
Space Scoop: www.unawe.org/kids/